



KAMPENI YA KITAIFA YA KUPIMA VVU NA KUANZA ARV MAPEMA

“FURAHA YANGU – PIMA, JITAMBUE, ISHI”

Dondoo za Kampeni wakati wa Vipindi vya Redio, Televisheni na Maigizo

1.0. Kampeni ya Furaha yangu – Pima Ishi Jitambue

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP) kwa kushirikiana na TACAIDS na Taasisi ya Mkapa kupitiana Amref Health Africa mradi wa Kifua Kikuu na UkimwiTB/HIVinatekelezakampeni ya Kitaifa ya **Kupima VVU na Kuanza ARV Mapema** inayo julikana kama **“Furaha Yangu, Pima, Jitambue, Ishi”**. Kampeni hii ambayo inasimamiwa na Wizara ya Afya kupitia NACP kwa kushirikiana na Amref kupitia mradi wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) unaolenga Ukimwi na Kifua Kikuu, katika hili mradi huu unaenda sambaba na maazimio ya kitaifa ya upimaji wa VVU chini ya kampeni iliyozinduliwa na **Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa (Mb)**, siku ya tarehe 19/06/2018 katika uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma.

Katika kuchangia juhudi za serikali na wadau mbalimbali wa masuala ya UKIMWI, Taasisi ya Mkapa kupitia Amref chini ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund), inatekeleza kampeni hii mikoa ya Arusha, Manyara, Tanga na Mtwara ambapo huduma ya kupima VVU, huduma ya tiba na Matunzo na huduma zingine za afya zitakuwa zikitolewa bila malipo.

2.0. Furaha Yangu inajumuisha

2.1. Umuhimu wa kupima na Kuanza ARV Mapema

Tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo mtu akipimwa VVU na kukutwa ameambukizwa alikuwa ahanzishiwi ARV hadi afikie kiwango furani cha CD4 ambapo watu wengine walipata magonjwa nyemelezi, hivi sasa utaratibu umebadilika, SASA ukipimwa na kukutwa umeambukizwa VVU utanzishiwa ARV mapema yaani ndani ya wiki mbili tu baada ya kushauriwa na mtoa huduma za afya.

Utaratibu huu umeleta mageuzi makubwa katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI nchini.

2.2. Faida ya kuanza ARV mapema ni pamoja na:

- Ukipima VVU na ukigundulika unamaambukizi unaanza kutumia





ARV mapema tofauti na zamani ambapo ililazimu kusubiri kiwango cha CD4.

- Siku hizi unatakiwa kutumia kidonge kimoja tu cha ARV kwa siku, tofauti na zamani MVIU alikuwa akilazimika kumeza vidonge nyingi.
- Kwa kuanza ARV Mapema utaimarisha kingamwili na kutoshambuliwa na magonjwa nyemelezi
- Ukizingatia matumizi sahihi ya ARV kiwango cha VVU mwilini kitashuka na kupunguza uwezekano wa kumwambukiza mwenza wako
- Iwapo umeambukizwa VVU unaweza kulinda Furaha yako tumia ARV kidonge Kimoja, Kila Siku, Muda na Wakati uleule
- ARV zinaondoka hofu ya kupoteza maisha kutokana na UKIMWI

Furaha Yangu – Pima Ishi, Jitambue, Ishi

2.3. Umuhimu wa wanaume Kupima

Kampeni ya Furaha yangu inahamasisha watu wote kupima VVU na kuanza ARV mapema kwa walio gundulika kuwa na VVU. Lakini kwa awamu hii ya kwanza tunawalenga wanaume zaidi kwa sababu takwimu za utafiti wa Viashiria vya VVU na UKIMWI nchini wa mwaka 2016-2017 umeonyesha kuwepo na kiwango cha chini cha upimaji wa VVU kwa wanaume ukilinganisha na wanawake. Inakadiriwa kuwa asilimia 48 ya watu wanaoishi na VVU Tanzania hawajui kuwa wana maambukizi ya VVU. Hali hii ni hatari kwa afya ya watu hao, familia, kaya na Taifa kwa ujumla.

Huduma

- Huduma za Upimaji wa VVU zinapatikana katika vituo vyote vyakutolea huduma za afya bila malipo na katika hudumamkoba zinazotolewa katika ngazi ya jamii, kama vile maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu n.k
- Huduma za tiba na matuzo zikiwemo ARV zinapatikana katika hospitali zote, vituo vya afya na baadhi ya zahanati bila malipo

Caption for Furaha yangu programs

Kipindi hiki kinadhaminiwa na kampeni ya **“FURAHA YANGU” PIMA, JITAMBUE, ISHI**

inayoletwa kwenu na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia NACP kwa kushirikiana na TACAIDS kwa hisani ya watu wa marekani pamoja na Mfuko wa Dunia (Global Fund).

